

Kucheza "Kuna Mlima wa Kijani Mbali"

Weka mikono yako kwenye kinanda ilivyoonyeshwa chini.

Tumia makundi mawili na matatu ya vibonyezo vyeusi ili kuku-saidia kupata mahali sahihi.

Cheza wimbo huu wa injili, ukifua-ta nambari za vidole kama ilivyoonyeshwa. Noti zilizo na ma-shina yanayoenda juu ni za mkono wa kulia, na noti zeny e shina manayoenda chini ni za mkono wa kushoto. Fanya mazoezi ya wimbo huu wa injili hadi uzoee. Tumia kanuni rahisi za mbinu za kubo-nyeza zilizoorodheshwa katika orodha ya hoja tisa.


Sasa umetambulishwa katika kucheza kinanda na umejifunza melodi rahisi ya wimbo wa injili. Kucheza nyimbo nyingine za injili, unahitaji kujifunza kanuni kadha za msingi kuhusu vipimo vya mu-ziki, sauti, na noti.

Hii ndiyo sehemu bora zaidi: somo ambalo umejifunza tu hivi sasa ni somo la kwanza katika Kozi ya Kiibodi ya Kanisa, inayopatikana katika lugha sita kutoka idara ya Kanisa ya Usambazaji.¹ Mpango huu wa maelekezo yaliyo rahisi kufuata unakusaidia kujifunza peke yako au kwenye vikundi. Unaweza hata kushirikisha famili-a yako nzima katika kujifunza

kucheza kinanda kama shughuli ya mukutano wa jioni ya familia nyumbani. Kozi hii inaweza ku-kamilishwa katika muda wa wiki sita tu.

Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa masomo ya muziki kibinagsi husaidia kuimarisha malengo ya wanafunzi, kuboresha msimamo wa kitaaluma na ujuzi wa kufikiri mambo yenye kujenga hoja.²

Kwa kujifunza ujuzi wa kucheza muziki, tunakuza vipaji ambavyo Mungu ametupa, tun-ongeza maarifa yetu, na kujifunza njia tofauti ambazo tunawenza kutumia maarifa na vipaji hivyo kujenga Ufalme wake. ■



MUHTASARI

1. Kuagiza Seti ya kujifunza kucheza kinanda nenda kwa store.lds.org
2. Tazama Laura Lewis Brown, "Manufaa ya Masomo ya Muziki," pbs.org; Jessica Velasco, "Jinsi Sanaa Inavyowezza Kuwasaidia Wanafunzi Kufanya Vizuri," the Science of Learning Blog, Dec. 11, 2012, scilearn.com/blog/how-arts-help-students-excel; "Muziki Unawasaidia Watoto Kujifunza Hesabu," The Telegraph, Mar. 22, 2012, telegraph.co.uk.